Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Agosti

# TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.09 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz




HALIUZWI

## Bima ya Kilimo ni Mkombozi kwa Wakulima

Wasiliana nasi coi@tira.go.tz | Au tupigie +255 222 132 537 | FB, IG, X: //@tira_tz

# Yaliyomo

03




08




01 TIRA na Konsotia ya Bima ya Kilimo Washiriki Maonesho ya Nanenane Dodoma, Elimu Bima ya Kilimo Yatolewa

02 TIRA NA CRDB Kuneemesha Sekta ya Kilimo

04 Viongozi Waandamizi wa ARCORP Kutoka Misri Watembelea Sekta ya Bima Tanzania

05 Ushirikiano Sekta ya Bima na Vyombo vya Habari Wadhihirika

06 Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Atembelea Banda la TIRA Maonesho ya Nanenane, Asisitiza Utoaji Elimu

07 Wakulima, Wafugaji na Wavuvi Wapewa Rai Kujiunga na Bima ili Kulinda Uwekezaji Wao Dhidi ya Majanga Yasiyotabirika

08 Nawapongeza kwa Juhudi Zenu, Ukuzaji Soko la Bima – Dkt. Saqware

09 Kazi na Afya: Watumishi TIRA Wakutana Pamoja, Washiriki Michezo Mbalimbali

10 TIRA Yadhamini na Kushiriki katika Tuzo za Ubora katika Sekta ya Mawasiliano 2025 Zanzibar

11 TIRA Yashiriki Maonesho ya Nanenane Kupitia Kanda ya Magharibi - Tabora

12 Nanenane Arusha: TIRA na Utoaji Elimu ya Bima, Makundi Mbalimbali Yanufaika

13 Elimu ya Bima Yatolewa kwa Wanafunzi wa Udereva Mwanza; Njia za Kidigitali Uhakiki wa Bima Zaelezwa

14 TIRA Nyanda za Juu Kusini Yaelimisha Umma kuhusu Bimakatika Maonesho ya Wakulima (Nanenane)



**Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

**Mhariri**
Hadija Maulid

**Waandishi**
Tabia Mchakama
Anna Massao

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba


TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRA Updates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Agosti 2025.





Scan
Kusoma Kidijiti

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
**info@tira.go.tz**

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
**www.tira.go.tz**

# TIRA na Konsotia ya Bima ya Kilimo Washiriki Maonesho ya Nanenane Dodoma, Elimu Bima ya Kilimo Yatolewa




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na Umoja wa Kampuni za Bima zinazotoa bima ya Kilimo (TAIC) walishiriki katika Maonesho ya Wakulima Nane Nane yaliyofanyika kitaifa mkoani Dodoma katika Viwanja vya Nzuguni,ambayo yalianza tarehe 1 Agosti na kumalizika Agosti 10, 2025.

Aidha, ushiriki huo ulilenga kutoa elimu ya bima pamoja na kuhamasisha wakulima, wafugaji na wavuvi kutumia huduma za bima ili kujikinga na athari za majanga yasiyotarajiwa.

Katika kipindi chote cha Maonesho, wananchi waliotembelea banda la TIRA na TAIC walipata nafasi ya kuelewa namna bima ya kilimo inavyoweza kusaidia kulinda mali zao dhidi ya changamoto mbalimbali kama vile ukame, mafuriko, magonjwa ya mimea na mifugo, pamoja na kushuka kwa uzalishaji.

Kwa upande wa Mamlaka, ilisisitiza kuwa bima ya kilimo ni kinga madhubuti inayowapa wakulima uhakika wa kurejesha mitaji yao na kuendelea na shughuli za uzalishaji hata pale majanga yanapotokea na kuwapa utulivu wa akili katika shughuli zao huku ikiimarisha ustawi wa sekta ya kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa.

# TIRA NA CRDB Kuneemesha Sekta ya Kilimo



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) na Benki ya CRDB zimekubaliana kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Bima ya Kilimo pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wanaohusika katika kuendesha bima hizo nchini ili kuleta neema na mustakabali mzuri wa sekta ya kilimo.

Hayo yameafikiwa Agosti 11, 2025 kwenye Kikao maalumu baina ya Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Bwn. Abdulmajid Nsekela kilichofanyika Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa Mazungumzo hayo Dkt. Baghayo Saqware amesema, Kutokana na hati ya ushirikiano (MoU) iliyosainiwa mwaka 2024 baina ya TIRA na CRDB kuhusu kufanya maboresho kwenye sera ya kilimo hakuna budi sasa kuanza utekelezaji wake kwakuwa MoU imebainisha wazi maeneo ya ushirikiano baina ya pande hizo mbili hivyo CRDB kuendelea kuwezesha mchakato.

Nae kwa upande wake Bwn. Abdulmajid Nsekela alisema, Benki ya CRDB ipo tayari kuendelea kutekeleza makubaliano ili kuleta tija kwenye kilimo na kwamba inatazamia kuwa na mchakato wa uwezeshaji katika uboreshaji wa Sera ya Kilimo ambao ni shirikishi.

Maeneo mahsusi yaliyobainishwa kwenye MoU hiyo ni pamoja na mageuzi ya sera, utengenezaji wa bidhaa za bima na kujengeana uwezo.





# Viongozi Waandamizi wa ARCORP Kutoka Misri Watembelea Sekta ya Bima Tanzania




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), tarehe 14 Agosti 2025 ilipokea ziara ya heshima kutoka kwa viongozi waandamizi wa kampuni ya ARCORP Holdings, kampuni ya kibiashara kutoka Misri inayojihusisha na masuala ya uwekezaji katika miradi mbalimbali, ikiwemo sekta ya bima. Ziara hiyo ilifanyika katika Ofisi Ndogo za TIRA jijini Dar es Salaam, ambapo wageni hao walipokelewa na Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo A. Saqware, pamoja na maafisa waandamizi wa TIRA. Kupitia ziara hiyo, ARCORP ilieleza dhamira yake ya kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza miradi ya kisasa itakayosaidia kuongeza ufanisi na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za bima nchini.

Aidha, ARCORP ilipata nafasi ya kufanya mazungumzo na Umoja wa Kampuni Waandikishaji wa Bima Tanzania (ATI), ambapo walibadilishana mawazo kuhusu fursa za kutumia mifumo ya kiteknolojia ili kuboresha huduma za bima na kuongeza uelewa kwa wananchi.

Kama sehemu ya mashirikiano yake, ARCORP pia inafanya kazi kwa karibu na wadau muhimu wa kitaifa wakiwemo Jeshi la Polisi Tanzania, Idara ya Uhamiaji, na Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (TISEZA), kwa lengo la kuhakikisha mshikamano mpana katika utekelezaji wa miradi yake nchini.
TIRA inatambua nafasi ya wawekezaji katika kuendeleza sekta ya bima na itaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha masoko ya bima nchini yanabaki salama, imara na yenye manufaa kwa wananchi wote.

# Ushirikiano Sekta ya Bima na Vyombo vya Habari Wadhihirika




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilikutana na Vyombo vya habari mbalimbali tarehe 18 Agosti 2025 jijini Dar es Salaam na kueleza mafanikio ya sekta ya bima chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Katika Mkutano huo ulioratibiwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, aliwasilisha Taarifa ya Maendeleo ya Sekta ya Bima kwa kipindi cha miaka minne (2021–2024) ambapo alielezea hatua kubwa zilizopatikana katika sekta hiyo ambapo Wahariri Zaidi ya 40 na Waandishi 50 walihudhuria mkutano huo.

Wakati wa uwasilishaji wa taarifa hiyo Dkt. Saqware aliwahimiza wahariri na vyombo vya habari kwa ujumla kuendelea kushirikiana na TIRA akisema kuwa vyombo vya habari vina nafasi ya kipekee ya kuwa daraja kati ya sekta ya bima na wananchi, na hivyo vina jukumu la kuhakikisha elimu ya bima inawafikia Watanzania wote kwa njia mbalimbali.

"Wanahabari mnapaswa kuwa wasemaji wabobezi wa masuala ya bima ili kuhakikisha jamii inapata taarifa sahihi na zenye kuaminika. Kupitia kalamu na majukwaa yenu mbalimbali , wananchi wataweza kuelewa nafasi ya bima katika maisha yao." Alisisitiza Dkt. Saqware

Kupitia mkutano huo na programu nyingine zilizoandaliwa na TIRA kwa wanahabari ni wazi kuwa ushirikiano kati ya sekta ya bima na vyombo vya habari utaendelea kuimarika na kuhakikisha mafanikio ya sekta ya bima yanapaziwa sauti na yanafahamika kwa Watanzania wote.

Vyombo vya habari vitabaki kuwa sehemu muhimu katika ukuaji wa sekta ya bima nchini, kwani ndio vinavyoiunganisha sekta hii na wananchi. Kwa ushirikiano wa karibu na endelevu, elimu ya bima itaendelea kutolewa ili wananchi washiriki zaidi katika sekta ya bima, na hatimae bima kubaki kuwa nguzo muhimu ya ustawi wa maendeleo ya Taifa.

# Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Atembelea Banda la TIRA Maonesho ya Nane Nane, Asisitiza Utoaji Elimu









Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Mhe. Mhandisi Athuman Kilundumya alitembelea mabanda ya TIRA na TAIC Maonesho ya Nane Nane Dodoma na kupongeza mafanikio uhamasishaji bima ya kilimo.

Aidha alitoa rai elimu hiyo ipelekwe zaidi kwa wakulima ili waweze kulinda mali zao kwa bima na kusisitiza utoaji elimu zaidi kwa wananchi ili wakulima, wafugaji na wavuvi waweze kutumia na kuongeza ujumuishi wa bima kwa wananchi wa hali zote wanaofanya shughuli hizo.

# Wakulima, Wafugaji na Wavuvi Wapewa Rai Kujiunga na Bima ili Kulinda Uwekezaji Wao Dhidi ya Majanga Yasiyotabirika




Rai hiyo ilitolewa na Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware wakati akizungumza na vyombo vya habari katika kilele cha Maonesho ya Nanenane na kuyataka makundi hayo kulinda mali zao kwa bima, alisema TIRA imelenga kutoa elimu nchi nzima kuhusu bima za kilimo ufugaji na uvuvi, hususan kipindi ambacho serikali inawekeza kupitia mpango wa BBT. Mathalani kwa sasa kampuni 15 zinatoa huduma za bima ya kilimo.

Akieleza faida ya bima kwa wakulima, Dkt. Saqware alisema kuwa tayari wapo ambao wameshanufaika na bima ya kilimo akibainisha kuwa mwaka 2023, wakulima wa tumbaku mkoani Tabora walilipwa zaidi ya shilingi bilioni mbili kutokana na hasara walizopata, fedha zilizotokana na mfuko wa pamoja wa kampuni za bima za kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Insurance na mwakilishi wa TAIC, Wilson Mzava, alibainisha kuwa umoja huo umeleta bima bora kwa bei nafuu na malipo ya haraka, huku ikipunguza mzigo wa kifedha kwa kampuni moja pale majanga yanapotokea.

Kwa upande wake, Msajili wa Migogoro ya Bima kutoka kwa Msuluhishi wa Migogoro ya Bima (TIO), Bw. Jamal Mwasha, amesema TIO inalinda maslahi ya watoa huduma na wateja wa bima kwa kutatua migogoro kwa njia mbadala, na aliwataka wananchi wasisite kuwasilisha malalamiko yao ili kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

# Nawapongeza kwa Juhudi Zenu, Ukuzaji Soko la Bima – Dkt. Saqware




Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware ametoa pongezi za dhati kwa Chama cha Mawakala wa Bima Tanzania (IAAT) kufuatia mchango wao kwenye kukuza sekta ya bima nchini.

Dkt. Saqware alitoa pongezi hizo wakati akisoma hotuba yake ya ufunguzi kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa IAAT Agosti 15,2025 jijini Dar es Salaam.

Aidha, Kamishna alisisitiza kuwa sekta ya bima ni mhimili muhimu wa ustawi wa kijamii na kiuchumi, na kusisitiza bima hutoa kinga dhidi ya majanga ya kifedha na huchochea uwekezaji, na kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania.

\Mawakala wa bima, kama daraja kati ya kampuni za bima na wananchi, wanabeba jukumu la kuhakikisha wananchi wanaelewa thamani ya bima, wanapata huduma kwa wakati, na kulindwa dhidi ya hatari mbalimbali.

Kupitia elimu ya bima wanayoipata, Dkt. Saqware aliwataka mawakala kuwa mabalozi wa kuhamasisha wananchi kuwekeza kwenye huduma za bima.TIRA itaendelea kuhakikisha sheria na kanuni zinalinda haki za watumiaji wa huduma za bima, kuhamasisha matumizi ya bima kwa sekta isiyo rasmi, na kutoa mafunzo na vyeti vinavyokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa kwa mawakala.

Alimalizia hotuba yake kwa kutoa wito kwa mawakala wa bima kuongeza uadilifu katika kazi, kujifunza ili kuendana na  mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya wateja, na kushirikiana kwa kutumia vyema jukwaa hilo kama chombo cha kubadilishana uzoefu na kujenga misingi imara ya ushirikiano.

# Kazi na Afya: Watumishi TIRA Wakutana Pamoja, Washiriki Michezo Mbalimbali



Mkoani Pwani wilayani Bagamoyo katika eneo lenye mandhari ya kuvutia na utulivu, lililozungukwa na miti na vichaka, ndipo watumishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) walipokutana na kufurahia tukio lililoacha kumbukumbu ya kipekee.

Tarehe 20 Agosti 2025, walitembelea eneo la Ndoto Polepole kushiriki michezo ya kujenga mwili na akili sambamba na kuimarisha mshikamano wao wa kikazi.

Shughuli hiyo ilihudhuriwa na uongozi wa juu, menejimenti pamoja na watumishi wa TIRA kutoka maeneo mbalimbali nchini. Kupitia michezo ya kutumia utashi, lengo likiwa ni kuongeza ushirikiano na kuboresha utendaji kazi. Aidha, michezo ya kufurahisha kama kuvuta kamba, kuendesha baiskeli na karata ilifanyika. Wafanyakazi wenye vipaji vya uchoraji, uimbaji na kucheza muziki nao walipata nafasi ya kuonyesha uwezo wao, ikilenga kuburudisha na kuonesha mshikamanano wa pamoja nje ya mazingira ya kazi.

Shughuli hizi zilifanyika mara baada ya Kikao cha Wafanyakazi 2025 kilichoandaliwa na Kurugenzi ya Utawala na Rasilimali Watu tarehe 19 Agosti 2025. Katika Kikao hicho, semina mbalimbali kuhusu uboreshaji wa ufanisi kazini na afya ya akili ziliendeshwa, kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi watumishi na kuongeza tija katika kuimarisha utendaji kazi wa taasisi hiyo.

# TIRA Yadhamini na Kushiriki katika Tuzo za Ubora katika Sekta ya Mawasiliano 2025 Zanzibar






Katika usiku uliosheheni shangwe, hamasa, na utambuzi wa ubora wa mawasiliano, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) iling'ara vilivyo — si kama mgeni tu, bali kama mdhamini na mshirika muhimu wa maendeleo ya taaluma ya mawasiliano nchini na kupata tuzo maalum.

Tuzo za Ubora wa Mawasiliano (Zanzibar Communication Excellence Awards - ZACEA) zilifanyika katika ukumbi wa Golden Tulip Hotel, tarehe 7 Agosti 2025 ambapo zilikutanisha wataalamu wa mawasiliano, Taasisi za Serikali, vyombo vya habari, kampuni za Mawasiliano, pamoja na wadau kutoka sekta binafsi na za umma kutoka Visiwani humo na Bara.

Mgeni Rasmi akiwa ni Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mhe. Shariff Ali Shariff. Lengo kuu la tukio hilo lilikuwa ni kutambua na kuenzi juhudi za ubunifu na ubora katika tasnia ya mawasiliano.

# TIRA Yashiriki Maonesho ya Nanenane Kupitia Kanda ya Magharibi - Tabora




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia ofisi zake za Kanda ya Magharibi ilishiriki kikamilifu katika Maonesho ya Kilimo ya Nanenane mwaka 2025 yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Ipuli, Jijini Tabora.

Kupitia ushiriki huo, TIRA iliendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa bima katika maisha yao ya kila siku, pamoja na mchango wake katika kulinda mali na kuboresha ustawi wa jamii.

Aidha, wananchi walipata nafasi ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi kuhusu huduma mbalimbali za bima nchini.

Elimu kwa makundi mbalimbali ya wananchi ilitolewa wakiwemo wakulima, wafanyabiashara, wanafunzi na wafanyakazi mbalimbali.TIRA imekuwa ikitumia majukwaa ya maonesho kama haya kuimarisha uelewa wa umma kuhusu masuala ya bima, sambamba na kutekeleza kauli mbiu yake ya "TIRA kwa Soko Salama la Bima."

# Nanenane Arusha: TIRA na Utoaji Elimu ya Bima, Makundi Mbalimbali Yanufaika




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kanda ya Kaskazini Arusha, ilishiriki Maonesho ya Wakulima yaliyofanyika katika viwanja vya Nane Nane Njiro jijini humo.

Maonesho hayo yalianza tarehe 1 Agosti na kumalizika Agosti 8, 2025. Lengo la ushiriki lilikuwa kutoa elimu ya bima. Agosti 3, 2025, banda la TIRA lilitembelewa na wanafunzi mbalimbali kutoka Young Boys Academy ambao walipewa elimu ya bima kwa kuelezwa umuhimu wa bima ikiwemo bima za afya na kuaswa kuwa mabalozi wazuri wa bima kwa wengine ili kukuza kizazi kinachofahamu umuhimu wa kuwa na kinga dhidi ya majanga.

Kwa upande mwingine, elimu kuhusu bima ya kilimo, uvuvi na ufugaji ilitolewa katika maonesho hayo kwa ajili ya kuhamasisha kukinga mali dhidi ya majanga kama ukame, mafuriko na wadudu waharibifu.

# Elimu ya Bima Yatolewa kwa Wanafunzi wa Udereva Mwanza; Njia za Kidigitali Uhakiki wa Bima Zaelezwa



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) kupitia Ofisi ya Kanda ya Ziwa, tarehe 26 Agosti, 2025 iliendesha mafunzo maalum ya bima kwa madereva wanafunzi zaidi ya 150 wa chuo cha VETA jijini Mwanza.

Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uelewa kuhusu umuhimu wa bima, hususan kwa madereva wapya wanaoingia kwenye sekta ya usafirishaji wa abiria na mizigo.
Kupitia mafunzo hayo, wanafunzi walipatiwa elimu ya aina mbalimbali za bima sahihi za vyombo vya moto.

Aidha, walifundishwa namna ya kuchagua bima stahiki kulingana na aina ya chombo cha moto na matumizi yake, jambo linalosaidia kupunguza migogoro na athari zinazoweza kujitokeza wakati wa majanga.
Mbali na hayo, TIRA pia iliwaelimisha washiriki kuhusu mchakato sahihi wa kuwasilisha madai ya bima pindi ajali au tukio la hatari linapotokea.

Vilevile, walifundishwa njia rahisi na za kidigitali za kuhakiki bima za vyombo vya moto ili kuepuka bima ghushi. Hatua hii inatarajiwa kusaidia kukuza nidhamu na uelewa wa bima miongoni mwa madereva na hivyo kuongeza usalama barabarani.

# TIRA Nyanda za Juu Kusini Yaelimisha Umma kuhusu Bima katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane)




Ofisi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilishiriki katika Maonesho ya 32 ya Wakulima Nane Nane yaliyofanyika katika Uwanja wa John Mwakangale, jijini Mbeya kuanzia Agosti 1 hadi 8, 2025.

Kupitia banda lake, TIRA ilitoa elimu kwa wananchi wa mkoa wa Mbeya na maeneo ya jirani kuhusu umuhimu wa bima mbalimbali ikiwemo bima ya afya, bima za vyombo vya moto, bima za ajali na nyinginezo. Msisitizo maalum uliwekwa kwenye bima za kilimo, ambapo wakulima walihamasishwa kuzitumia ili kulinda mali zao na kujiandaa dhidi ya majanga yanayoweza kuathiri uzalishaji.

Maonesho hayo yalikuwa fursa muhimu kwa TIRA kuendelea kuhamasisha wananchi kuelewa na kutumia huduma za bima kama kinga ya kiuchumi na kijamii.

# Majibu ya Maswali yako Kuhusu Bima

*Pata majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara*



## Bima ni nini?

Bima ni mkataba wa kisheria kati ya pande mbili yaani kampuni ya bima na mtu binafsi, kikundi au kampuni (mbima), ambapo kampuni ya bima inaahidi kulipa fidia iwapo janga lililokatiwa bima litatokea na kusababisha hasara. Hivyo, bima ni nia ya kuhamishia majanga kwa kampuni za bima na kupata kinga dhidi ya majanga mbalimbali yasiyotarajiwa. Bima hukatwa kwa ajili ya kukinga majanga mbalimbali yanayotuzunguka kila siku.

## Majanga ni nini?

Ni hatari yeyote isiyotabirika inayoweza kusababisha upotevu wa fedha, maisha na mali. Hatari hizi zinaweza kutokea katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kila siku. Hivyo, matukio kama ajali za vyombo vya usafiri, moto, mafuriko, magonjwa, ukame ni baadhi tu ya majanga yanayoweza kumkumba mwananchi.

## Bima ina umuhimu gani kwa mali na maisha ya mwananchi?

Bima ni muhimu kwani inahakikisha usalama wa kukabiliana na aina yoyote ya changamoto maishani. Bima ni sehemu muhimu sana katika mipango ya mwananchi katika uwekezaji wa kiuchumi na kijamii.

## Je, ni nani anastahili kuwa na Bima?

Bima ni nyenzo muhimu sana kwa kila mwananchi, hivyo hakuna anayebaguliwa ama kupewa kipaumbele sana katika kupata huduma za bima.

Hii ni kwa sababu kila mmoja kwa wakati fulani hukumbwa na janga aidha la kiuchumi (kupata hasara katika Biashara, kilimo, ufugaji n.k) na kijamii (yaani kuuguliwa, kufiwa na hata watoto kukosa ada na chakula n.k). Hivyo, kuzingatia aina hii ya uwezekano wa kupatwa majanga, jamii yote huhitaji bima za aina mbalimbali kulingana na uhitaji.

## Ni nani aliyepewa dhamana ya kutoa huduma za Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, Soko la Bima nchini linasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo hutoa leseni kwa kampuni za bima ambazo hubeba dhamana ya kutoa fidia kwa wananchi waliokata bima.

Pia, wananchi wanaweza kupata huduma za bima kupitia Washauri na Madalali wa Bima, Mawakala wa Bima kupitia Benki na Mawakala wa Bima waliosajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuna watoa huduma za bima wanaosajiliwa na Mamlaka kama Wakadiria Hasara, Wakaguzi Binafsi na Wakala wa Ufuatiliaji wa Fidia.

## Ni wakati gani Bima inahitajika?

Bima inahitajika mara tu unapokuwa hauna uhakika na uwezekano wa kuwa katika hali yako ya awali iwapo janga litakupata. Hivyo, ni vema ikafahamika kuwa bima hukatwa mapema ili kujikinga na janga kabla halijatokea. Iwapo itakatwa baada ya janga kutokea haitofaa kutoa fidia kwa janga lililopita.

## Je, ni lazima kuwa na Bima?

Kimsingi, mwananchi anawajibika kukinga mali na wapendwa wake kwa hiari yake kwa kuwakatia bima. Pamoja na hiari hiyo, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya Mwaka 1973, iliyorekebishwa 2002 imewapasa wamiliki wa vombo vya moto wanaotumia barabara za umma kukata bima ndogo (Third Party Insurance) ili kumkinga mtu wa tatu dhidi ya majanga yanayosababishwa na vyombo vya moto.

## Je, ni nani mnufaika wa Bima?

Bima hunufaisha wamiliki wa bima au wakata (policyholders) na wahanga kulingana na aina

ya bima iliyokatwa na majanga yaliyosababisha hasara. Kwa mfano, Bima za Maisha na Bima za Afya hunufaisha mkataji bima ama wanufaika walioandikwa katika mkataba wa bima.

Kwa upande wa Bima za Muda Mfupi, mnufaika wa kwanza huwa ni mkata bima hususan kwenye bima za moto, kilimo, ajali, biashara, n.k. Bima ndogo (Third Party) hunufaisha moja kwa moja mtu wa tatu aliyesababishiwa janga iwe kuumizwa yeye mwenyewe ama kuharibiwa mali zake.

## Mkata bima ana wajibu katika suala zima la kupata huduma za Bima?

Ni kweli kuwa mkata bima anao wajibu katika hatua za kukata bima na wakati bima iko hai.

Wakati wa kukata bima atawaibika kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa ukweli usiyo na shaka (bila kuongopa), kujaza fomu ya uhitaji wa bima na kutaja wanufaika (hii ni kwa Bima za Maisha na Bima za Afya), kuwa na nyaraka zote muhimu wakati wa ukataji bima kabla ya kuchukua mkataba wa bima; kufanya madai kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa bima na kufuata mchakato wa madai.

## Je, pindi mkata bima anapopatwa na janga, ni wapi anatakiwa kutoa taarifa?

Pindi janga lililokatiwa bima linapotokea mkata bima mwenye mkataba wa bima anapaswa kutoa taarifa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga dhidi ya mali yake ili kuwezesha hatua zingine za fidia kuendelea. Utaoaji wa taarifa uzingatie taratibu zilizowekwa katika mkataba wa bima. Inashauriwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 baada ya janga kutokea.

Mhanga anaweza pia kutoa taarifa kwa wakala au dalali wa bima aliyemkatia bima. Lakini isisahaulike kuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na ngazi mbalimbali za Serikali, kwa mfano: inapotokea ajali, mkata bima atoe taarifa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani au nyumba inapoungua ni vema kutoa taarifa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa upande mwingine kuna Ofisi za Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata.

Kutoa taarifa sehemu zote hizi hujenga msingi mzuri wa mkata bima kufidiwa bila mashaka ya tukio kwani linakuwa limehakikiwa na ngazi husika.

## Ni muda gani umewekwa kwa kampuni kushughulikia fidia kwa mhanga wa ajali au kuharibikiwa na mali iliyowekewa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, kampuni ya bima inapaswa kushughulikia madai ya wateja kwa muda mfupi kulingana na ukubwa wa janga na uthibitisho wa janga lenyewe kuwa halali. Baada ya kujiridhisha kuwa janga hilo ni sahihi na kutoa hati ya kukubali janga, kampuni itawajibika kutoa fidia kwa mteja ndani ya siku zisizozidi 45.

## Ni jinsi gani mteja anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ndicho chombo cha Serikali kinachowajibika kumlinda mteja wa bima (mkata bima). Hivyo, ni sahihi kabisa

kwa mnufaika wa huduma za bima kuleta lalamiko lake dhidi ya huduma za bima anazopewa na kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa TIRA kupitia barua pepe au simu, kutegemea uko eneo gani nchini. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko kupitia tovuti: www.tira.go.tz ambapo utajaza fomu ya malalamiko na kuiwasilisha.

## Je, kuna tofauti kati malalamiko ya Bima na migogoro ya Bima?

Malalamiko ya bima ni tofauti kigodo na migogoro ya bima, kwani malalaiko ya bima hutokana na huduma hafifu zinazotolewa na watoa huduma wa bima kwa wananchi waliosajiliwa na Mamlaka na mara nyingi aina hii ya malalamiko uhusisha wahanga wa ajali (third party) na haya huwasilishwa kwa Kamishna wa Bima kwa hatua stahiki.

Migogoro ya bima ni ile inayohusisha mteja kutokubaliana na kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Migogoro hii hupelekwa kwenye Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) kwa hatua zaidi.

## Je, kuna Bima kwa ajili ya kilimo na mifugo?

Soko la Bima nchini linaendelea kukua kila siku. Aina mbalimbali za bima zinatolewa ikiwemo Bima za Kilimo naBima za Mifugo. Bima ya Kilimo hukatwa kwa ajili ya kukinga moto, mafuriko, ukame, wanyama na wadudu waharibifu. Kwa upande wa Bima ya Mifugo, hutolewa kwa ajili ya kukinga magonjwa, upotevu na vifo.

## Je, TIRA ina mifumo yoyote ambayo inaitumia katika usimamizi wa shughuli za Bima kwenye soko?

Ndiyo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina mifumo mingi katika utoaji wa huduma za bima: Mafno: Mfumo wa TIRA-MIS unaotumika kukata bima na kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto na mali za mteja, mfumo mwingine ni Tanzania Import Insurance Portal (TIP) kwa ajili ya bima za mizigo kutoka nje ya nchi kwa njia meli (bahari) na dege (anga).

Pia mfumo wa Risk Based Supervision (RBS) kwa ajili ya upokeaji wa taarifa na uchambuzi wa viashiria vya majanga. Mifumo hii yote imeunganishwa na taasisi stahiki za Serikali pamoja na watoa huduma za bima.

## Je, ninaweza kuhakiki bima ya chombo cha moto na mali zangu?

Ndio, unaweza kuhakiki bima yako kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.

## Je, Kuna Bima kwa ajili watu wa kipato cha chini?

Ndio. Ipo bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini, bima hii hufahamika kama "'microinsurance'. Ni bima ndogo ambayo ni kwa ajili ya kumkinga mtu asiyeweza kuingia kwenye utaratibu wa bima yenye gharama kubwa kutokana na kiwango cha fedha anachokipata.

Mfano kwa wale wanaofanya shughuli za uJulainga, mama/baba lishe, na wengine wenye biashara ndogo ndogo. Bima hizi hulipa fidia endapo mbima atapata hasara kwenye biashara yake aliyoikatia bima.



# TIRA & 2025


**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

**FB, IG, X:** //@tira_tz
www.tira.go.tz